DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME
PROGRAMA DEL DIPLOMA

# Swahili – Souahéli – Suaheli

## *Ab Initio*

### Language-Specific Syllabus
### Programme Spécifique
### Programa de Estudios Específico

IBO
INTERNATIONAL BACCALAUREATE
BACCALAURÉAT INTERNATIONAL
BACHILLERATO INTERNACIONAL

*Language* ab initio – *Langue* ab initio – *Lengua* ab initio

*September 2002 – Septembre 2002 – Septiembre de 2002*

For first examinations in 2004

Premiers examens en 2004

Primeros exámenes en 2004

© International Baccalaureate Organization 2002

Organisation du Baccalauréat International
Route des Morillons 15
Grand-Saconnex / Genève
CH-1218
SWITZERLAND

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Lesikoni 1 | 2 |
| Mtu Binafsi na Wengine | 2 |
| Elimu na Kazi | 3 |
| Miji na Huduma | 4 |
| Chakula na Vinywaji | 5 |
| Burudani na Kusafiri | 6 |
| Mazingira | 7 |
| Afya na Huduma za Dharura | 8 |
| Lesikoni 2 | 9 |
| Silabasi/Muhtasari wa Sarufi | 12 |
| Masuala Mahsusi Kuhusu Lugha na Ufundishaji wa Kiswahili | 27 |
| Utaratibu na Maelekezo ya Maswali ya Mitihani | 28 |

# Utangulizi

Hali mbalimbali na mada za mawasiliano ambazo zimeorodheshwa katika mwongozo wa *ab initio* katika maelekezo ya silabasi au muhtasari huu ndizo msingi mkuu wa kozi hii ya *ab initio.*

Muhtasari mahsusi wa lugha unaorodhesha msamiati na kutoa maelezo kuhusu vipengele vya sarufi ambavyo mwanafunzi atahitaji kuvijua ili kuweza kufikia malengo ya lugha katika kiwango cha *ab initio*.

- Mwongozo wa Lugha Mahsusi una sehemu zifuatazo:
- Maelekezo ya lesikoni (lexical guide)
- Muhtasari au silabasi ya sarufi
- Utaratibu na maelekezo kuhusu mitihani
- Masuala mahsusi kuhusu lugha ya Kiswahili na ufundishaji wake.

## Maelekezo ya Lesikoni

Mwongozo wa Lesikoni **unagusia** juu ya aina ya msamiati ambao utawaruhusu na kuwawezesha wanafunzi kuwasiliana katika hali mbalimbali za kila siku. Mwongozo huu umegawanywa katika sehemu mbili: Lesikoni 1 na Lesikoni 2.

Katika **Lesikoni 1** mfano wa msamiati umeonyeshwa kwa kila mada kuu na mada ndogo ya Silabasi Kuu. Mifano hii inarejelea nyanja pana za misamiati ambazo hazina budi kufundishwa ili kumwezesha mwanafunzi akamilishe mahitaji ya mawasiliano kufuatana na kila mada. Hii itakuwa kama hatua ya kuanzia kwa ajili ya mwalimu ambaye anatarajiwa kwamba atachagua msamiati zaidi kufuatana na mahitaji na mambo wanayopenda kuyaongelea wanafunzi wake.

**Lesikoni 2** inatoa msamiati wa ziada kwa kuorodhesha muhtasari wa vitenzi, vihusishi na viunganishi, nambari, nchi na majina yake, mahali, umbali, kueleza saa/wakati, majira mbalimbali, siku za juma/wiki, miezi na tarehe.

## Muhtasari/Silabasi ya Sarufi

Sehemu hii ina vipengele vya sarufi ambavyo watahiniwa watahitaji kuvijua ili kuweza kuwasiliana kwa Kiswahili katika hali mbalimbali za kila siku, lakini pia ili waweze kujibu maswali ya mitihani ya kuandika na kuzungumza.

Ni muhimu kwamba sarufi iunganishwe na ufundishwaji wa sehemu zingine za kozi hii.

## Masuala mahsusi kuhusu Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii ina habari ambazo ni mahsusi kuhusu lugha ya Kiswahili na ufundishaji wake.

## Utaratibu na Maelekezo Kuhusu Mitihani

Sehemu hii ina mifano ya maelekezo ambayo aghalabu hutumiwa katika maswali ya mitihani ya kiwango hiki cha lugha hii. Orodha hii ni ya mifano tu wala haijakamilika, na baadhi ya maelekezo katika mtihani wenyewe huweza kuto kutofautiana na haya kufuatana na mahitaji ya huo mtihani.

# Lesikoni 1

## Mapendekezo ya Msamiati

### Mtu Binafsi na Wengine

#### HABARI BINAFSI

| | |
|---|---|
| Anuani na Habari | jina, umri, jinsia, umeoa/umeolewa? Utaifa, mahali unakoishi: barabara au |
| Nyingine Binafsi | mtaa, jina la mji au jiji, namba ya simu, n.k. |
| Watu na vikundi vya watu | mtoto, watoto, rafiki, mikutano, shirika lako… |
| Familia | ndugu (mama/baba mkwe, mtot pekee…) sherehe mbalimbali (siku za kuzaliwa, kumbukumbu za harusi, n.k. |
| Salamu/Kuamkiana | hujambo, sijambo, habari gani, nzuri, habari za…kazi, masomo… |

#### SURA, NAMNA UNAVYOONEKANA, NA MAVAZI

| | |
|---|---|
| Sura/Namna Unavyoonekana | mrefu, mfupi... (macho) rangi...nywele (ndefu, fupi...) uzito… |
| Nguo/Mavazi | shati, sketi, suruali…; kuvaa…; mavazi rasmi, nguo za mirabamiraba… |
| Tabia | mcheshi, mzungumzaji, mwenye machachari… |
| Hisia | kuwa na matumaini, kufurahi...; kucheka, kutabasamu... |

#### NYUMBA/NYUMBANI

| | |
|---|---|
| Makazi | Aina ya nyumba (flati, nyumba ya kawaida, ghorofa…); baba au mama mwenye nyumba, mtunza nyumba…; kuhamia, kukodisha, malipo… |
| Maelezo kuhusu nyumba | vyumba (bafuni, chooni…); ghorofani, sebuleni, juu, karibu…; samani au fenicha (vitanda, meza, viti, makochi…); vyombo vya nyumbani na vya jikoni (friji, jiko…); nje (ukuta/kuta, paa…); bustani (mimea, majani, maua…); mazingira mazuri, nafasi kubwa/ndogo… |
| Vitongoji | viambazani, kijiji, majumba mengi, kelele, ukimya… |
| Ratiba/Mazoea | kuamka, pupiga mswaki…; kuwahi, kuchelewa…; siku za juma; kusema saa (alfajiri, mchana, jioni, usiku, usiku wa manane, saa mbili saubuhi…); tarehe…; mara kwa mara, kila mara, mara mojamoja… |
| Majukumu nyumbani | kusaidia, kuandaa meza, kupiga pasi…; kutunza/kuangalia wanyama (mbwa, paka…) |
| Mialiko | kukaribisha, kukataa…; kutembelea; kadi, barua, barua-pepe/ i-meli…; kuwa na nafasi, kuwa nashughui nyingi… |
| Misemo muhimu | karibu/karibuni!, samahani, unaonaje?… |

# Elimu na Kazi

## SHULE

| | |
|---|---|
| Shule, wanafunzi, waalimu | msingi, sekondari, ya serikali, binafsi…; mwanafunzi, kidato cha tano…; mwalimu mkuu wa shule, mkufunzi… |
| Majengo na Nyenzo | darasa, viwanja vya michezo… |
| Vifaa vya darasani | kitabu, tepu rekoda, redio, televisheni, video… |
| Kompyuta | disketi, kipanya…; kuwasha/kuzima, kudaunlodi…; intaneti, barua-pepe, i-meli, faksi… |
| Programu za taaluma | masomo (mazingira, historia…); Istilahi za IB (Diploma, kiwango cha juu, kiwango cha kati…); kazi ya nyumbani…; shughuli za darasani (kujadili, kueleza, kufafanua…; neno, aya, mstari…); mawazo binafsi (mazuri, yenye maana…); mitihani (kufaulu, kushindwa/kufeli…); ratiba (kipindi, mapumziko ya chakula cha mchana, michezo…) |
| Shughuli nje ya masomo au nje ya darasa | ubunifu (sanaa…) Michezo, Huduma kwa jamii; vyama (kwaya, klabu au chama cha kupanda milima…) |
| Kalenda ya shule | Siku ya michezo, likizo, ziara… |
| Kauli na maneno muhimu | kwa mawazo yangu, kwa upande mwingine, kinyume chake, nionavyo… |

## MIPANGO YA BAADAYE

| | |
|---|---|
| Studies | kujiandikisha…; chuo kikuu, shahada…; kazi…; malengo…; kozi ya wakati wa kiangazi |
| Utaalamu/Ubingwa | mwalimu, daktari, mwandishi wa habari… |
| Kazi/Ajira | maombi ya kazi, maelezo binafsi ya mtu (C.V.)…; kuajiriwa, kulipwa msharaha…; masharti (-a kudumu, -a muda…); bosi, mfanyakazi mwenzio…; tangazo la kazi… |
| Uzoefu wa kazi | mhudumu, msaidizi... |

# Mji na Huduma

## KUNUNUA VITU MADUKANI

| | |
|---|---|
| Aina za maduka | vifaa vya ujenzi, spea za magari, saluni za nywele…; soko, supamaketi, kibanda, grosari… |
| Dukani | sehemu, lifti, chumba cha kupimishia, kaunta ya kulipia…; mteja, mlaji, mhudumu…; ghorofa ya kwanza/pili…; mfuko, kigari…; bei, kujaribisha… |
| Bidhaa/ Vitu vya kununua | bidhaa (filamu, zawadi za kumbukumbu…); zimetengenezwa kwa (pamba…); saizi, aina…; rahisi, ghali, bidhaa bora…; punguza bei, badilishana…; malipo (bei, risiti, kadi…) |
| Misemo/Kauli muhimu | seli…; kodi ya vat, kodi ya ushuru?… |

## HUDUMA ZA JAMII NA MAWASILIANO

| | |
|---|---|
| Huduma za usafiri | basi, treni…; mahali pa kuegeshea magari; tiketi, njia, ratiba, tiketi, mashine, halali… |
| Benki/Banki | pesa, hundi za kusafiria, noti…; mashine ya pesa (ingiza kadi…); viwango vya kubadilisha pesa, hundi… |
| Posta | stempu/stampu, bahasha…; kutuma…; kwa ndege, paseli, kupokea |
| Simu | mwito wa mbali, piga/ita…; namba, dairektori, simu ya bure… |

# Chakula na Vinywaji

## KUNUNUA VITU MADUKANI

| | |
|---|---|
| Maduka ya vyakula | duka la mikate, grosari, supamaketi, marikiti, soko… |
| Pa kununulia mboga na matunda | nyama; samaka; matunda; mbogamboga, mboga za majani; kinywaji/vinywaji; idadi, uzito (kopo, fungu, robo kilo…) |

## KULA CHAKULA HOTELINI

| | |
|---|---|
| Aina za hoteli/ Migahawa | hoteli, mgahawa… |
| Hotelini/Mgahawani | menu/menyu/orodha ya vyakula; kufanya buking, mhudumu/ weita, tipu… |

## CHAKULA

| | |
|---|---|
| Mlo na vyakula | nyama choma, bankweti, chakula cha jioni, chakula cha mchana…; piza, kuku wa kuchoma/kukaanga…; tamu, -enye chumvi… |
| Resipe/Mahitaji | mahitaji (unga, sukari…); vyombo (bakuli, frangpeni, sahani…); njia/namna ya kuandaa (kukoroga, kukatakata, kuyeyusha…) |
| Kula nyumbani | chombo/vyombo, glasi, sahani…; kuandaa meza…; chumvi, pilipili, sosi… |
| Mlo/Maakuli | bila nyama, chakula cha Kiafrika/Kitanzania/Kikenya/Kihindi…; kalori, lishe… |
| Vyakula | chakula cha sherehe (keki ya bethdei/siku ya kuzaliwa…); vyakula vya kitaifa (pilau, ugali, steki, ndizi…) |
| Kauli/Misemo muhimu | karibuni, asante, bila asante, kwa afya/chiazi!... |

# Burudani na Kusafiri

## BURUDANI NA STAREHE

| | |
|---|---|
| Shughuli za kujifurahisha | kukusanya stempu…; kufurahia…; riwaya, tamthilia, shairi (mwandishi, mhusika, sura, hadithi ya kubuni…) |
| Vyombo vya Habari | televisheni (stesheni, kipindi, katuni…); redio (taarifa ya habari); habari (gazeti, gazeti la kila wiki, kichwa cha habari, makala…) |
| Michezo | soka, kandanda…; timu; kushinda, kushindwa…; kufundisha, mazoezi, mechi…; mtazamaji, mpenzi/shabiki wa timu… |
| Burudani | konseti, senema, video, pati, mwigizaji, bendi, kwaya, maonyesho…; kuulizia, tiketi… |
| Maoni | -a kusisimua, -a kuchekesha, nzuri sana…; kuchukia, kuchosha, kupendelea… |

## MAZINGIRA

| | |
|---|---|
| Sehemu mbalimbali | kanisa, msikiti, bwawa la kuogelea, viwanja vya michezo, bustani za kupumzikia… |
| Maelekezo ya njia | kiplefti, barabara kuu…; karibu, ng'ambo, kushoto, kulia…; kugeuka, kupinda, kukata, kukatisha… |
| Maneno/ Kauli muhimu | umbali wa mita mia moja, nusu kilomita… |

## LIKIZO NA KUSAFIRI

| | |
|---|---|
| Usafiri | kufanya buking (chumba cha mtu mmoja/watu waili, selfu kontein…); ratiba, njia…; kondakita, abiria…; ofisi ya tiketi, mzigo uliopotea…; kuondoka, kuwasili, kubadili, uwanja wa ndege, pasi/pasipoti/hati ya kusafiria, forodha… |
| Shughuli | mpango wa safari, kupanda mlima, ziara…; sherehe, maadhimisho…; kutembelea, kujianika juani, kuogelea, kufurahia mazingira… |
| Maulizo kuhusu likizo | ofisi ya habari kwa wataliiwakala wa safari…; kijitabu cha maelekezo, gazeti, bango…; ratiba…; kituo cha mwisho… |

## MALAZI

| | |
|---|---|
| Aina za malazi | hoteli, hosteli, bweni, hema/mahema… |
| Vifaa, nyezo na kufanya buking | chumba cha watu wawili (dabo), upatikanaji, kuwasili…; kujiandikisha… |
| Sheria/Masharti | usegeshe gari hapa, usivute sigara, wageni hawaruhusiwi vyumbani, usipige kelele… |

# Mazingira

## HALI YA HEWA

| | |
|---|---|
| Hali za hewa | kunyesha…; ukungu…; utabiri wa hali ya hewa, nyuzijoto $20^{o}$… |
| Misimu | baridi…; kipupwe, kiangazi, masika, vuli… |
| Misimu zaidi | mvua fupi, mvua ndefu…; kuvuna, jua kali… |

## JIOGRAFIA YA MAZINGIRA

| | |
|---|---|
| Mazingira ya kijiografia | mlima, ufukweni/bichi, volkano, maporomoko, jangwa… |
| Nchi na mikoa au sehemu zake | kaskazini, kusini, mashariki, magharibi…; jiji, mji mkuu, mikoa, wilaya, miji, vijiji… |

## MASUALA YA MAZINGIRA

| | |
|---|---|
| Ikolojia | uchafuzi wa mazingira (mvua ya tindikali, takataka…); kurudufu bidhaa; maliasili (maji, umeme, misitu, mito, maziwa…) |
| Masuala ya kimataifa | viumbe walioko hatarini kupotea, Umoja wa mataifa, vita, wakimbizi… |

# Afya na Huduma za Dharura

## AFYA

| | |
|---|---|
| Magonjwa na kuumia | sehemu za mwili; goti lililoteguka, kikohozi, mafua, kuumwa kichwa…; inauma, bandeji, plasta; kutibu…; kusumbuliwa na…, kupona… |
| Miadi/Ahadi ya kuonana | kuweka ahadi, kuahirisha…; kliniki, X-rey…; daktari wa meno, kujaza jino; daktari wa watoto, nesi… |
| Dawa na kuandikiwa dawa | vidonge, krimu, duka la madawa…; matone matatu, kutwa mara tatu, baada ya chakula… |
| Maneno muhimu | usife moyo, ugua pole, upone, tunakutakia afya njema, pole sana… |

## DHARURA

| | |
|---|---|
| Kuibiwa na kupoteza kitu | umbo, ukubwa/saizi, size, maelezo…; polisi, ubalozi, mali iliyopotea, jinai, uhalifu, kosa, wizi…; taarifa/ripoti, bima… |
| Ajali | ambulesi/ambalanzi, shahidi, moto, tetemeko la ardhi…; huduma ya kwanza, kuzama, kufa maji, kuokoa… |
| Matengenezo/Ripea | kuharibika, vunja, pasua, gongana, huduma ya kwanza, dharura… |
| Alama/Mabango | hatari, usiingie, usipite hapa, ujenzi unaendelea… |

# Lesikoni 2

## Muhtasari wa Vitenzi

1. vya kawaida (imba, cheka, andika, rudi, soma, sema...)
2. vifupi (-la, -nywa, -ja, -fa, -wa, -enda, -nya...)

## Vihusishi na Viunganishi

| | |
|---|---|
| **ajili** | kwa ajili ya, kwa ajili yangu... |
| **baada ya** | baada ya kazi, baada ya kusoma... |
| **badala ya** | badala yangu, badala ya kulala... |
| **bila ya** | |
| **chini ya** | chini yangu... |
| **dhidi ya** | |
| **juu ya** | juu ya hayo, juu yangu/yako/yake/yetu/yenu/yao... |
| **kabla ya** | kabla ya kulala, kabla yangu, kabla ya saa sita... |
| **kadiri ya** | kadiri unavyotaka |
| **kando** | kando ya, kando yangu... |
| **karibu** | karibu watu wote, karibu ya/na... |
| **kati** | kati ya... |
| **katika** | katika utawala wake... |
| **katikati ya** | |
| **kiasi cha** | kiasi cha ku, kiasi unachotaka |
| **kijuujuu** | |
| **kimsingi** | |
| **kuhusu** | |
| **kutokana na** | |
| **kwa:1** | kwa kuwa, kwa sababu, kwa sababu ya, kwa vile, kwa vipi?<br>kwa vyovyote vile |
| **kwa:2** | kwangu, kwako, kwake, kwetu, kwenu, kwao |
| **kwenye** | |
| **licha ya** | |
| **mbali** | mbali na hayo, mbali na nyumbani... |
| **mbele** | mbele ya, mbele ya Mungu, mbele yangu... |
| **mkono wa** | mkono wa kushoto/kulia |
| **moja kwa moja** | |
| **ndani** | ndani ya, ndani yake |
| **ng'ambo** | ng'ambo ya... |
| **nje** | |
| **tangu** | |
| **upande** | upande wa kushoto, kulia... |
| **wakati wa...** | |
| **yaani** | |
| **zaidi** | zaidi ya, zaidi ya haya/hayo... |

## Nambari

| | | |
|---|---|---|
| moja mbili tatu | kumi na moja...ishirini | tisini |
| nne tano | ishirini na moja...thelathini | mia |
| sita | arobaini | mia moja na moja |
| saba | hamsini | mia mbii |
| nane | sitini | mia tatu...elfu moja |
| tisa | sabini | elfu mbili...laki moja |
| kumi | themanini | laki mbili...milioni/ bilioni/trilioni... |
| mtu **m**moja | sita | kumi na mmoja |
| watu **wa**wili | saba | kuma na wawili... |
| **wa**tatu | **wa**nane | ishirini na mmoja |
| **wa**nne | tisa | ishirini na Wawili... |
| **wa**tano | kumi | watu thelathini/ arobaini... |
| kiti kimoja | mti mmoja...mitatu... | kalamu tatu |
| viti viwili...viti | nyumba/kalamu | nne |
| sita... | moja | tano |
| | mbili | sita... |
| mtu wa kwanza | kiti cha kwanza | mti wa kwanza |
| mtu wa pili | kiti cha pili | mti wa pili |
| mtu wa tatu | kiti cha tatu | mti wa tatu |
| mtu wa nne.... | kiti cha nne..... | mti wa nne... |
| kalamu ya kwanza | ukuta wa kwanza | mahali pa kwanza |
| kalamu ya pili | ukuta wa pili | mahali pa pili |
| kalamu ya tatu | ukuta wa tatu | mahali pa tatu |
| kalamu ya nne... | ukuta wa nne... | mahali pa nne... |

## Nchi

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania | Urusi | Ureno |
| Kenya | Uingereza | Misri... |
| Marekani | Ujerumani | |
| lugha ya Kiswahili | lugha ya Kirusi | lugha ya Kijerumani |
| lugha ya Kichina | lugha ya Kiingereza | lugha ya Kipare... |
| chakula cha Kitanzania | chakula cha Kireno | chakula cha Kiyahudi... |
| chakula cha Kirusi | | |

## Mahali

pa/kwa/mwa
kwangu, kwako, kwake, kwetu, kwenu, kwao…
pangu, pako, pake, petu, penu, pao, tazama sehemu ya Sarufi

## Umbali

| | | | |
|---|---|---|---|
| kilomita | maili | mita | yadi |

## Kueleza saa/Wakati

| | | |
|---|---|---|
| saa | saa mbili/tatu | kasoro dakika ishirini |
| dakika | saa moja na dakika tano | kasoro robo/kasa robo |
| nukta | saa...na robo | kamili |
| saa moja | saa...na nusu/u nusu | |

### Nyakati

| | | |
|---|---|---|
| alfajiri | alasiri | jioni |
| asubuhi na mapema, | adhuhuri | usiku |
| asubuhi | mchana | usiku wa manane… |

## Majira

| | | |
|---|---|---|
| vuli | jua | kilimo |
| masika | kiangazi | kupanda |
| majira/wakati/kipindi | rasharasha | kuvuna |
| mvua | kipupwe | |

## Siku za juma/Wiki

| | | |
|---|---|---|
| Jumatatu | Jumatano | Ijumaa |
| Jumanne | Alhamisi | Jumamosi |
| | | Jumapili |

## Miezi

| | | |
|---|---|---|
| Januari | Mei | Septemba |
| Februari | Juni | Oktoba |
| Machi | Julai | Novemba |
| Aprili | Agosti | Desemba |

Pia: mwezi wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano…

## Tarehe

siku ya…tarehe moja mwezi wa kwanza mwaka wa elfu moja mia tisa na tisini na tisa, mwaka wa elfu mbili na moja…

# Silabasi/Muhtasari wa Sarufi

## Silabi, Sauti na Matamshi

### Msamiati wa Matamshi

### Irabu

A E I O U

Irabu huonyesha mwisho wa silabi.

Matamshi husisitiza silabi ya pili kutoka mwisho.

**Maneno ya silabi mbili**

| | |
|---|---|
| nani | na/ni |
| tuko | tu/ko |

**Maneno ya silabi tatu**

| | |
|---|---|
| barua | ba/ru/a |
| teua | te/u/a |

**Maneno ya silabi nne**

| | |
|---|---|
| anataka | a/na/ta/ka |
| nimesema | ni/me/se/ma |
| fikiria | fi/ki/ri/a |

**Neno lenye silabi 14**

wa/ta/ka/o/no/ng'o/ne/za/na/no/ng'o/ne/za/na

## Konsonati

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **b** | babu | barabara | **n** | nani | nunua |
| **ch** | chacha | chuchu | **p** | popo | papa |
| **d** | dudu | dadisi | **r** | radi | rarua |
| **f** | fifia | fafunua | **s** | sasa | sisi |
| **g** | gogo | garagara | **t** | tatua | totoa |
| **h** | hati | hohehahe | **v** | vivi | vuvia |
| **j** | jaji | jambo | **w** | wewe | waya |
| **k** | kuku | kaka | **y** | yeye | yaya |
| **l** | lulu | lalamika | **z** | zeze | zoza |
| **m** | mema | mimina | | | |

## Zingatia matamshi yafuatayo ambayo yanachanganya konsonanti (Special Consonant Combinations)

**-ch**agua
**dh**ambi
**dh**ana
**dh**ima
**gh**ali
**gh**arika
ki**my**a
mara**dh**i
**mbw**a
**nd**oo
**-ng'**a**ng'**ania
**ng'**ombe
**nj**e
**nz**ima
se**ng'**enge
**tha**mani
**th**ela**th**ini
**thu**muni

## Maneno marefu

a t a k a y e n i n u n u l i a
wanaonong'onezananong'onezana

## Sauti za M na N

Sauti hizi mbili za **m** na **n** zenyewe ni SILABI, na huweza kutokea mwanzoni mwa neno iwapo hakuna irabu zinazozifuatia.

### Sauti za M hutamkwa midomo ikiwa imefungwa

| | |
|---|---|
| m ta ro | m t u |
| m me a | m t o |
| m p a na | m t i |
| m s o m a j i | m b u |

### Sauti za N

| | |
|---|---|
| n c h i | n n e |
| n d i y o | n t a |
| n g e | n z u r i |
| n g u v u | |

## Silabi Pacha

**aa ee ii oo uu**

### Sema maneno haya:

| | |
|---|---|
| aongee | mguu |
| choo | mkuu |
| hasikii | sambaa |
| kondoo | utembee |
| kufaa | utii |

Vilevile, silabi pacha huweza kupatikana mwanzoni au hata katikati ya maneno kama vile:

| | |
|---|---|
| andaaandaa | kaakaa |
| gaagaa | keekee |

# Nyakati/Tensi

| + | LI | ME | NA | TA |
|---|---|---|---|---|
| - | KU | JA | -i- | TA |
| | -NGALI- | | | |
| | -NGE- | | | |

## Wakati uliopita: LI

Ni**li**lala mapema.
U**li**soma kitabu cha Kiswahili.
A**li**ongea na wageni.

Tu**li**sherehekea Krismasi nyumbani.
M**li**kula chakula kizuri hotelini.
Wa**li**kunywa bia za Tanzania.

## Wakati uliopita hivi karibuni: ME

Ni**me**lala mapema.
U**me**soma kitabu cha Kiswahili.
A**me**ongea na wageni.

Tu**me**sherehekea Krismasi nyumbani.
M**me**kula chakula kizuri hotelini.
Wa**me**kunywa bia za Tanzania.

## Wakati uliopo: NA

Ni**na**lala mapema.
U**na**soma kitabu cha Kiswahili.
A**na**ongea na wageni.

Tu**na**sherehekea Krismasi nyumbani.
M**na**kula chakula kizuri hotelini.
Wa**na**kunywa bia za Tanzania.

## Wakati ujao: TA

Ni**ta**lala mapema.
U**ta**soma kitabu cha Kiswahili.
A**ta**ongea na wageni.

Tu**ta**sherehekea Krismasi nyumbani.
M**ta**kula chakula kizuri hotelini.
Wa**ta**kunywa bia za Tanzania.

## Past conditional: NGALI

Ni**ngali**lala mapema…
U**ngali**soma kitabu cha Kiswahili…
A**ngali**ongea na wageni…

Tu**ngali**sherehekea Krismasi nyumbani…
M**ngali**kula chakula kizuri hotelini…
Wa**ngali**kunywa bia za Tanzania…

## General conditional: NGE

Ni**nge**lala mapema…
U**nge**soma kitabu cha Kiswahili…
A**nge**ongea na wageni…

Tu**nge**sherehekea Krismasi nyumbani…
M**nge**kula chakula kizuri hotelini…
Wa**nge**kunywa bia za Tanzania…

## Kukanusha Nyakati

| | | |
|---|---|---|
| **KU** | Ni**li**lala | Si**ku**lala |
| **JA** | Ni**me**lala | Si**ja**lala |
| **i** | Ni**na**lala | Silal**i** |
| **TA** | Ni**ta**lala | Si**ta**lala |
| **SINGE** | Ni**nge**lala | Ni**singe**lala |
| **SINGALI** | Ni**ngali**lala | Ni**singali**lala |

# Ngeli za Majina

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | M: | mtu | Wa: | watu |
| 2 | M: | mti | Mi: | miti |
| 3 | Ki: | kiti | Vi: | viti |
| 4 | Ji: | jani | Ma: | majani |
| 5 | N: | nyumba | N: | nyumba |
| 6 | U: 1 | uongo | U: 1 | uongo |
| 7 | U: 2 | ukuta, ulimi | U: 2 | kuta, ndimi |
| 8 | U: 3 | ugonjwa | U: 3 | magonjwa |
| 9 | Ku: | kuimba | Ku: | kuimba |
| 10 | Mahali:<br>Mahali:<br>Mahali: | pa<br>ku/kwa<br>mu/mwa | Mahali:<br>Mahali:<br>Mahali: | pa<br>ku/kwa<br>mu/mwa |

## Ngeli ya M-Wa

Uundaji wa vitenzi katika ngeli za M-Wa kwa nyakati zote:

| | | |
|---|---|---|
| Ni | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |
| U | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |
| A | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |
| Tu | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |
| M | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |
| Wa | + li/me/na/ta/ngali/nge | + kitenzi |

## Vitenzi vifupi

| | | |
|---|---|---|
| -fa | ni + li/me/na/ta/ngali/nge | + kufa |
| -la | u + li/me/na/ta/ngali/nge | + kula |
| -ja | a + li/me/na/ta/ngali/nge | + kuja |
| -nywa | tu + li/me/na/ta/ngali/nge | + kunywa |
| -wa | m + li/me/na/ta/ngali/nge | + kuwa |
| -enda | wa + li/me/na/ta/ngali/nge | + enda |

## Tungo Kanushi za Wakati Uliopo

| | |
|---|---|
| Si | Sitaki chai. |
| Hu | Huta**ki** kahawa? |
| Ha | Hauliz**i** swali? |
| Hatu | Hatujibu maswali. |
| Ham | Hamsem**i** Kiingereza. |
| Hawa | Hawatok**i** Uingereza. |

Katika kukanusha wakati uliopo, vitenzi vifupi havitumii **ku**:

**Mifano:**

Sili.
Huendi.
Haji.
Hatufi.
Hamnywi maji.
Hawawi madaktari.

## Kutumia KU katika Vitenzi

Kwenye vitenzi viwili au zaidi, kitenzi cha Kwanza hakitumii **ku**, lakini vinavyofuatia hutumia **ku**.

**Mifano:**

Ninataka **ku**lala.
Huwezi **ku**sema Kirusi.
Hataki **ku**la samaki wala **ku**nywa soda.
Tunataka **ku**la, **ku**nywa, **ku**nya (vulgar), **ku**furahi na **ku**lala.

## Vivumishi vya Kuonyesha

| | |
|---|---|
| huyu | yule |
| hawa | wale |

## Vivumishi vya Sifa na Idadi

| | |
|---|---|
| **m**zuri | **mw**embamba |
| **wa**baya | **wa**nene |
| **m**kubwa | **mw**eusi |
| **wa**dogo | **w**eupe |
| **m**refu | **m**moja |
| **wa**fupi | **wa**wili |
| | **wa**chache… |

## Vighairi (Exceptions)

**-ingi** **-ingine** **-ote**

Vivumishi hivi vina matumizi maalumu na tofauti.
Kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| Badala ya | "watu **wa**ingi" | = "watu wengi" |
| Badala ya | "mahali **pa**ingine" | = "mahali pengine" |

Mifano ya matumizi ya –ote:

sisi sote
ninyi **ny**ote
wao **w**ote

Hata hivyo, badala ya kutumia **s**ote au **ny**ote, kimatumizi, wasemaji na wazungumzaji wengi wanatumia tu **w**ote.

## Vivumishi vya Kumiliki: 1

| | |
|---|---|
| wangu | wetu |
| wako | wenu |
| wake | wao |

## Vivumishi vya Kumiliki: 2

yangu/yako/yake...n.k.
zangu/zako/zake...n.k.

Baadhi ya nomino zinazotumia vivumishi vya kumiliki (Vimilikishi) vya **Y** na **Z**.

Hizi ni nomino au majina yanayoshughulikia mahusiano ya kinasaba ya watu. Majina haya ni yale ambayo umoja na wingi wake ni sawa.

**Mifano:**

dada
baba
mama
bibi
babu
jirani
rafiki…n.k.

## Vighairi (Exceptions):

Kuna baadhi ya nomino ambazo zina wingi wa **WA** lakini hutumia vimilikishi vya **Y** na **Z**. Kwa mfano:

wake zangu/zako/zake/zetu/zenu/zao
wajomba zangu/zako/zake/zetu/zenu/zao

Baadhi ya nomino kama **jirani**, **rafiki**, **adui**, n.k. huweza kuwa na wingi wa **maj**irani, **ma**rafiki, **ma**adui n.k. ijapokuwa vimilikishi vyake vinabaki kuwa vya **Z**.

## Vivumishi vya Kulinganisha

kuliko
kuliko…-ote
kupita
zaidi ya
afadhali
kama
kabisa
mno
sawa na...n.k.

## Nyuso mbalimbali za kitenzi cha -WA (KUWA)

1. ni
2. si
3. kuwa
4. li na si: ni**li**ye - ni**si**ye

**Mfano:** Baba yetu uliye mbinguni

| Kuwa na… | Tungo Kanushi za Kuwa na… (Kutokuwa na): |
|---|---|
| Nina | Sina |
| Una | Huna |
| Ana | Hana |
| Tuna | Hatuna |
| Mna | Hamna |
| Wana | Hawana |

## Kuwa mahali (KO/PO/MO)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| niko | uko | yuko | tuko | mko | wako |
| nipo | upo | yupo | tupo | mpo | wapo |
| nimo | umo | yumo | tumo | mmo | wamo |

## Tungo Kanushi za (KO/PO/MO) (Kutokuwa mahali)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| siko | huko | hayuko | hatuko | hamko | hawako |
| sipo | hupo | hayupo | hatupo | hampo | hawapo |
| simo... | humo | hayumo | hatumo | hammo | hawamo |

| Kuna | Pana | Mna |
|---|---|---|
| Hakuna | Hapana | Hamna |

## Nyakati (LI-ME-NA-TA-HU-NGE-NGALI)

### Uliopita (LI)

Nililala
Nilikuwa na njaa

### Tungo Kanushi (KU)

Sikulala
Sikuwa na njaa

### Timilifu (ME)

Umesoma
Umekuwa na…

### Tungo Kanushi (JA)

Hujasoma
Hujawa na…

### Ujao (TA)

Ataimba
Atakuwa na njaa

### Tungo Kanushi (TA)

Hataimba
Hatakuwa na njaa

### Kila Wakati (HU)

Sisi hunywa maji
Sisi huwa na…

### Tungo Kanushi (Kama NA)

Sisi hatunywi maji
Sisi hatuwi na…

### NGE/NGALI

Mngecheza
Wangaliona
Ningekuwa na pesa nyingi ninge...

### Tungo Kanushi (SINGE na SINGALI)

Msingecheza
Wasingaliona
Nisingekuwa na pesa nyingi nisinge…

## Matumizi ya Vitenzi Vifupi kwa Nyakati Zote

| Kitenzi | Tungo isiyo kanushi | Tungo kanushi |
|---|---|---|
| -ja | **Ninakuja** sasa hivi. | **Siji** sasa hivi. |
| -la | **Umekula** chakula? | **Hujala** chakula? |
| -wa | **Alikuwa** mgonjwa. | **Hakuwa** mgonjwa. |
| -fa | **Tutakufa**. | **Hatutakufa**. |
| -nywa | **Mngekunywa** maji. | **Msingekunywa** maji. |

## -PO (when) na Tungo Kanushi ya -SIPO

Kwa kuweka **-po** baada ya kiashiria wakati na kabla ya kitenzi:

| | |
|---|---|
| Nina**po**lala ninaota. | Ni**sipo**lala sioti. |
| Nili**po**soma nilifurahi. | |
| Nitaka**po**maliza shule nitalala. | Nisi**po**maliza shule (kesho) sitalala. |

## Maagizo

1. Kwa mtu mmoja:

| | |
|---|---|
| Lala! | Usila**le**! |
| Kunywa! | Usi**nywe**! |

2. Kwa mtu zaidi ya mmoja:

| | |
|---|---|
| Lal**eni**! | Msilale! |
| Kunyw**eni**! | Msinywe! |

3. Maalumu:

| | |
|---|---|
| Njoo! | Njoo**ni**! |
| Lete! | Lete**ni**! |
| Nenda! | Nend**eni**! |

## Ngeli Nyingine za Majina na Upatanisho Wake wa Kisarufi

Fuata mada za Ngeli za M-Wa kama zilivyoonyeshwa hapo juu, kwa ngeli zifuatazo:

| | |
|---|---|
| M | Mi |
| Ji | Ma |
| Ki | Vi |
| N | N |
| U | |
| Ku | |

Pa/Kwa/Mwa (pamoja na maneno kama: hapa, pale, huku, kule, humu, mle, humo, huko, hapo...)

## Viambishi vya Nafsi (Subject/Object Pronouns)

### M-WA

| | |
|---|---|
| -ni | Ana**ni**ona. |
| -ku | Tuna**ku**penda. |
| -m/mw | Wana**m**taka/Wana**mw**ona. |
| -tu | Mna**tu**chukia? |
| -wa...eni | Nita**wa**andiki**eni** barua. |
| -wa | Uta**wa**fundisha Kiswahili? |

### M-MI

| | |
|---|---|
| u–i | Tume**u**angusha mti. Wame**i**vuka mito. |

### JI-MA

| | |
|---|---|
| li–ya | Wana**li**fahamu jambo. Mna**ya**ona magari? |

### KI-VI

| | |
|---|---|
| ki–vi | Ata**ki**nunua kitabu hiki. Tuta**vi**uza vitu vile. |

### N-N

| | |
|---|---|
| i–zi | Ume**i**andika barua? Tume**zi**la ndizi. |

### U-U-N-MA

u–u–zi–ya

### P/K/M

| | |
|---|---|
| Pa/ku/mu | Nina**pa**ona pale mahali...n.k. |

### Kiambishi cha nafsi cha -JI kwa ngeli zote

Nina**ji**somea kitabu.
Ana**ji**penda sana.
Mlango ume**ji**funga.
Mtoto ame**ji**chafua.
Chakula kime**ji**ozea.

## Baadhi ya Kauli za Kitenzi

### Kauli ya Kutendwa (The Passive Form of the Verb)

| | |
|---|---|
| -piga | -pig**w**a |
| -penda | -pend**w**a |
| -pika | -pik**w**a |

### Kauli ya Kufanyiza (The Causative Form of the Verb)

| | |
|---|---|
| -safi | -safi**sha** |
| -penda | -pend**eza** |
| -soma | -som**esha** |
| -ingia | -ingi**za** |

### Kauli ya Kutendewa (Prepositional Form of the Verb)

| | |
|---|---|
| -soma | -som**ea** |
| -pika | -pik**i**a |
| -sema | -sem**ea** |
| -tembea | -tembe**le**a |
| -nunua | -nunu**li**a |

### Kauli ya Unafsi-Tisti (The Stative Form of the Verb)

| | | |
|---|---|---|
| -funga | -fungika | (closable) |
| -fungua | -funguka | (openable) |
| -penda | -pendeka | (lovable) |

## Matumizi ya -KI

-ki hutumika kama -po lakini kwa maana ya tendo lililokuwa linafanyika wakati lingine linafanyika vilevile, yaani kama Present Participle.

**Mifano:**

| | |
|---|---|
| Nilikuona u**ki**cheza. | I saw you play**ing.** |
| Tulikuwa tu**ki**imba. | We were sing**ing**. |
| Aliniangalia ni**ki**zungumza. | He watched me talk**ing**. |
| Tutawaona wa**ki**oana. | We shall see them marry**ing**. |
| Tutaonana Mungu a**ki**penda. | We shall see each other, God will**ing**. |

## Matumizi ya -AMBA

**-amba** katika ngeli zote za majina:

| | | |
|---|---|---|
| Mtu amba**ye** | Watu amba**o** | Mtu ambaye anafundisha... |
| Mti amba**o** | Miti amba**yo** | Mti ambao umeanguka... |
| Jina amba**lo** | Majina amba**yo** | Jina ambalo tunalipenda... |
| Kiabu amba**cho** | Vitabu amba**vyo** | Kitabu ambacho nilikisoma... |
| Nyumba amba**yo** | Nyumba amba**zo** | Nyumba ambayo ni nzuri... |
| Kalamu amba**yo** | Kalamu amba**zo** | Kalamu ambayo imepotea... |
| Ukuta amba**o** | Kuta amba**zo** | Ukuta ambao umeanguka... |
| Uhuru amba**o** | - | Uhuru ambao tumeupata... |
| Ubaya amba**o** | Mabaya amba**yo** | Ubaya ambao nimefanyiwa... |
| Mahali amba**po** | Mahali ambapo ni pazuri... | |
| Mahali amba**ko** | Mahali ambako si kwangu... | |
| Mahali amba**mo** | Mahali ambamo amejificha... | |

## Njia ya Pili

| | |
|---|---|
| Mtu ana**ye**fundisha | Watu wana**o**fundisha... |
| Jina tuna**lo**lipenda | Majina tuna**yo**(ya)penda... |
| Kitabu nili**cho**kisoma | Vitabu tuli**vyo**(vi)soma... |
| Mwaka uli**o**pita | Miaka ili**yo**pita... |
| Mwezi una**o**kuja | Miezi ina**yo**kuja... |

## Njia ya Tatu

| | |
|---|---|
| Mtu afundisha**ye** | Watu wafundisha**o**... |
| Jina tulipanda**lo** | Majina tuyapenda**yo**... |
| Mwezi uja**o** | Miezi ija**yo**... |

## -NDI ya kusisitiza

katika ngeli zote za majina:

| | |
|---|---|
| Huyu **ndiye** mwalimu wetu wa Kiswahili | Hawa **ndio** walimu wetu... |
| Huu **ndio** mti wa matunda. | Hii **ndiyo** miti... |
| Hili **ndilo** gari zuri. | Haya **ndiyo** magari... |
| Hiki **ndicho** kiti cha babu. | Hivi **ndivyo** viti... |
| Hii **ndiyo** nyumba yangu. | Hizi **ndizo** nyumba... |
| Huu **ndio** ugonjwa usumbuao. | Haya **ndiyo** magonjwa... |
| Huu **ndio** ukuta wa nyumba. | Hizi **ndizo** kuta... |
| Huku **ndiko** kuimba kuzuri. | - |
| Hapa **ndipo** nilipozaliwa. | - |
| Huku **ndiko** nilikosomea. | - |
| Humu **ndimo** alimojificha Osama. | - |

## Misemo mbalimbali kwa kutumia neno PIGA

| | |
|---|---|
| piga miayo | piga gitaa |
| piga piano | piga pasi |
| piga simu | piga gumzo |

## Methali na Nahau za Kiswahili: Utangulizi

| | |
|---|---|
| Maana<br>Matumizi<br>Maudhui<br>Fani | Mwalimu na wanafunzi watumie mifano mbalimbali ya methali za Kiswahili kwa kuzingatia maana za methali hizo, matumizi yake, maudhui na fani ya methali hizo. |

**Mifano ya methali:**

Haraka haraka haina baraka.
Mtaka cha uvunguni sharti ainame.
Usipoziba ufa utajenga ukuta.
Moyo wa mtu ni msitu.
Samaki mkunje yungali mbichi.
Usione vyaelea, vimeundwa!

**Mifano ya misemo/nahau:**

Alikuwa amewaka/amepiga maji/amechapa maji = Alikuwa amelewa.
Ana mkono wa birika = Ni bahili, hana ukarimu.
Msichana yule ni malaika = msichana yule ni mzuri...

# Masuala Mahsusi Kuhusu Lugha na Ufundishaji wa Kiswahili

## Matamshi na Kiimbo

Lugha ya Kiswahili haina utata sana kuhusu matamshi na kiimbo; lakini ni muhimu mwalimu anapofundisha lugha hii atilie mkazo katika masuala haya kwani yanaweza kuleta tofauti ya maana kutegemeana na neno linalotumika. Mathalani, kama inavyoonyeshwa katika sehemu inayohusu silabi, katika lugha ya Kiswahili silabi ya pili kutoka mwisho ndiyo inayosisitizwa katika kutamka baadhi kubwa ya maneno. Lakini pia mwalimu aeleze jinsi ambavyo maneno machache ya Kiswahili hayafuati kanuni hii. Hapa anaweza kutumia mifano ya manenoa kama vile:

- barabara kwa maana ya "vizuri"
- ghafla
- maktaba n.k.

Maneno haya hufuata kanuni za matamshi ya lugha yalikotoka.

## Upatanisho wa Kisarufi

Kwa miaka michache ambayo lugha hii imefundishwa katika kiwango hiki cha *ab initio* tatizo kubwa ambalo limeathiri sana matokeo ni lile la udhaifu katika upatanisho wa kisarufi. Ni muhimu sana sana kwamba mwalimu na wanafunzi wafanye mazoezi mengi kuhusu suala hili ili wanafunzi wajue kuwa kila kundi la nomino (ngeli ya majina) huwa na upatanisho wake wa kisarufi katika sentensi. Labda itakuwa vizuri kwa mwalimu kuanza na sentensi fupifupi na kuonyesha upatanisho huo, halafu jinsi muda unavyokwenda mwalimu azirefushe sentensi hizo kutoa vielelezo vya upatanisho zaidi. Mathalani, mwalimu anaweza kuanza na sentensi ya "Mwalimu mzuri" halafu akaendelea hatua kwa hatua kama ifuatavyo:

1. Mwalimu ni mtu mzuri.
2. Mwalimu wangu ni mtu mzuri.
3. Mwalimu wangu yule ni mtu mzuri.
4. Mwalimu wangu yule mzuri na mwembamba ni mtu ambaye hufundisha vizuri pia...n.k.

## Lugha ya Ishara na Tofauti za Kitamaduni

Katika ufundishaji wa lugha hii, pia ni muhimu mwalimu awajulishe wanafunzi kuhusu lugha ya ishara miongoni mwa wasemaji wa Kiswahili, na aonyeshe tofauti za lugha hii ya ishara na lugha za namna hii katika tamaduni zingine. Mathalani, mwalimu anaweza kuonyehsa kuhusu kukataa, kumwita mtu, kumuaga mtu, kumkubalia mtu, n.k. Hii lugha ya ishara huweza kumaanisha jambo moja katika utamaduni mmoja na kumaanisha jambo jingine, tena labda kinyume kabisa, katika utamaduni mwingine. Iwapo kuna video ambazo zinaweza kuonyeshwa darasani kwa ajili hii itakuwa vizuri sana. Haya na masuala mengine ya kiutamaduni wa Kiswahili husaidia sana kulifanya somo liwavutie na kuwafurahisha wanafunzi.

# Utaratibu na Maelekezo ya Maswali ya Mitihani

Ifuatayo ni mifano ya maswali/mazoezi ambayo yanaweza kutokea katika mitihani.

Karatasi ya Kwanza

- Kwa kutumia habari uliyosoma katika kifungu hiki, andika muhtasari wa mambo muhimu ambayo...
- Jibu maswali yafuatayo.
- Angalia fomu hiyo hapo chini halafu jibu maswali.
- Maneno ya Orodha A yamepigiwa mistari katika habari uliyosoma. Kwa kila neno tafuta maana iliyotolewa katika Orodha B kama ilivyotumika kwenye habari uliyosoma. Mfano umetolewa katika jibu la kwanza. Uwe mwangalifu kwa sababu Orodha A ina maelezo mengi kuliko maneno ya orodha A.
- Chagua jibu sahihi zaidi kati ya A,B,C na D; halafu andika herufi ya jibu hilo kwenye kisanduku kando ya swali.
- Angalia picha hizi usome habari iliyoko kando ya picha, halafu jibu maswali.
- Malizia sentensi zifuatazo kufuatana na habari uliyosoma.
- Kati ya sentensi zifuatazo kuna sentensi za kweli **(K)** na za uongo **(U)** kufuatana na habari uliyosoma. Zisome sentensi hizo halafu weka alama ya **K** kwenye kisanduku cha sentensi ya kweli na alama ya **U** katika kisanduku chenye sentensi isiyo ya kweli. Thibitisha jibu lako.
- Onyesha ni katika aya ipi unaweza kupata mawazo yafuatayo katika habari uliyosoma.
- Picha/sentensi zifuatazo zinatoa muhtasari wa habari uliyoisoma. Andika herufi inayoambatana na kila aya. Mfano umetolewa mwanzoni.
- Vichwa vya habari vya kila aya ya kifungu ulichosoma vimeorodheshwa hapo chini. Patanisha kila kichwa cha habari na aya inayohusika. Uwe mwangalifu kwa sababu kuna vichwa vingi vya habari kuliko aya zenyewe.
- Habari uliyoisoma ni ya mahojiano, lakini maswali/majibu ya mahojiano hayo hayapo. Maswali/majibu hayo yameorodheshwa hapo chini. Kwa kila jibu/swali chagua swali/jibu lake. Uwe mwangalifu kwa sababu kuna maswali mengi kuliko yanayohitajiwa.
- Kwa kila neno lililoorodheshwa hapo chini tafuta neno lingine lenye maana sawa na hilo kutoka katika habari uliyosoma sasa hivi.
- Katika habari ifuatayo kuna maneno yaliyoachwa. Yajaze maneno hayo kutoka katika orodha iliyotolewa chini yake. Kila neno litumiwe mara moja tu.
- Soma maelekezo yafuatayo halafu chora mishale ya kuonyesha njia ya kufuatwa katika ramani hiyo hapo chini.

Karatasi ya Pili

- Andika barua/faksi/telegramu/i-meli/barua-pepe kuhusu...
- Andika postikadi kuhusu...
- Andika tangazo kuhusu sherehe ya...shuleni kwenu.
- Andika shajara (kijitabu cha kumbukumbu/dayari) kuhusu safari au wiki unayoikumbuka kuliko zote.